# LEARNING BY EAR

## ”WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA DHIDI YA MALARIA”

## KIPINDI CHA TANO: "KINGA NI BORA KULIKO TIBA "

**SCRIPT: CHRISPIN MWAKIDEU**

**EDITOR: ANDREA SCHMIDT**

**ASSISTANT EDITOR: KATRIN OGUNSADE**

**HEATH EXPERT: DR.HEIDRUN HÜBNER**

**List of characters for episode 5:**

- MASIKA (40)
- BETTINA (34)
- KAREMBO (14)
- ZAWADI (BABY, no actor)
- MIZANJA/WITCHDOCTOR (65)
- DR. MUNGA (45)
- DUTY NURSE (24)
- YAKUBU (41)

**INTRO/NARRATOR**

Hujambo msikilizaji na karibu tena katika kipindi cha Noa Bongo Jenga maisha yako ambapo tunaendelea na mchezo wa kuigiza kwa jina WAGENI VIZABIZABINA **MSOALIKWA' VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA**. Katika kipindi kilichopita, karembo alikosa kwenda shuleni kwa wiki kadhaa kutokana na kuugua Malaria na David akatumwa kwenda kumjulia hali. Kwengineko, mama David alimshauri mamake karembo aende akamuone mganga kuhusu kuugua kwa karembo na kakake zawadi, yote haya yalikuwa kinyume na matakwa ya Masika, je, betina atafanyaje? Na karembo atayabaini haya? Tega sikio katika kisa **"KINGA NI BORA KULIKO TIBA"**

**MUSIC INTERLUDE.**

**<u>SCENE ONE: DR. MUNGA SLEEPING IN HIS HOME.</u>**

**A-SFX: HEAVY SNORING, FOLLOWED BY A SHARP MOBILE RINGTONE**

1. **DR. MUNGA:** **(AWAKE)**
Naam.. Daktari Munga hapa...

2. **DUTY NURSE:** **(URGENT)**
samahani daktari... pole kwa kukuamsha.. huyu mkunga wa zamu na tunakuhitaji kwa dharura hapa hospitali...tafadhali njoo haraka!

3. **DR. MUNGA:** Kuna dharura gani tena? Si nimetoka huko hivi punde? Kwani hakuna madaktari wengine wakaishughulikia dharura hiyo?

**4. DUTY NURSE:** Wote wameshikika kikazi... idadi ya wagonjwa imekuwa marudufu... Daktari. unafahamu kuwa takriban asilimia sitini ya idadi ya vitanda vimelaliwa na wagonjwa wa malaria.. na bado wagonjwa wanazidi kufurika... tumepokea mgonjwa ambae anaonekana bado mtoto mdogo hivi sasa ....

**5. DR. MUNGA:** Hali yake iko namna gani?

**6. DUTY NURSE: :** Hali yake?..eeh ni msichana mdogo ambaye anaonekana dhaifu, amedhoofu hivi kwamba hawezi hata kutembea bila kusaidiwa..

**7. DR.MUNGA:** Sawa,mchukuwe vipimo vyake vya joto, mfanyie utafiti wa damu tujue kama ana malaria nami niko njiani naja... nipe dakika ishirini...

**8. DUTY NURSE:** Harakisha basi..alafu bado jambo moja bwana daktari...

**9. DR. MUNGA:** **(TAKES DEEP BREATH)**
Sawa.. nakusikiliza

**10. DUTY NURSE:** Samahani lakini sijui kuchunguza damu yenye malaria.. nafahamu tu kutumia maikroskopu...au kipima vimemea lakini...

**11. DR. MUNGA:** **(CUTS HER SHORT)**

Nitamfanyia tafiti nikifika.. mchukuwe vipimo vya joto na ujaaribu kulimiliki joto lake lishuke chini.....

**12. DUTY NURSE:** Asante daktari tunakusubiri kwa hamu.

**NARRATOR:** Msikilizaji,Basi hayo na mengineyo kwa mfano uhaba wa vifaa na wataalamu wenye ujuzi wa kuitambua malaria kwa haraka ni moja ya sababu inayofanya vita hivi dhidi ya malaria kuwa vigumu…..Idadi kubwa ya waliofariki kutokana na maradhi hayo ingelinusurika iwapo tungelipata vifaa na wataalamu katika mahospitali yetu... basi Daktari Munga alipokuwa tayari anafulizia hospitali, betina naye alikuwa anaelekea kwa mganga mizanja akiwa kambeba zawadi mgongoni na karembo anamfuata asijuwe aendako wala yatakayomsibu...

**<u>SCENE TWO: ON WAY TO MIZANJA THE WITCHDOCTOR'S SHRINE</u>**

**13. B-SFX: FOOTSTEPS ON PATH WALKING SLOWLY**

**14. KAREMBO:** Mama.. kwani twaenda wapi? Hujasema chochote tangu tulipotoka nyumbani.. najionea kwenda tu, na twendako hatufiki...

**15. BETTINA:** Wewe huniamini? Mazungumzo ya nini na nguvu zenyewe huna? Kazana twende bado tuko na safari..

**16. KAREMBO:** Wajuwa david alinieleza nini?

**17. BETTINA:** **(UNPLEASANTLY)**
hapana Karembo, nitajuwaje aliyekueleza na ni

wewe ndiye uliyezungumza na yeye..
(**FEELS SORRY FOR SICK DAUGHTER)**
pole mwanangu... enhe, alikwambia nini?

**18. KAREMBO:** Alinieleza kuwa mwalimu mkuu aliwaeleza jinsi ya kuondosha mbu mbali. Alisema kuwa kukata nyasi zilizozingira nyumba zetu, kuondosha maji yaliyokikangama karibu na nyumba zetu na tukifanya hivyo hawa wageni wetu wasioalikwa wataondoka na kushindwa kutaga mayai yao.

**19. BETTINA:** (**NOT ATTENTIVE)**
Hmm..sawa.

**20. KAREMBO:** Basi baada ya mazungumzo nikipata wazo..

**21. BETTINA:** Wewe unaugua!inafaa utafakari kupona kwako kwa sasa sio mambo yasio na msingi...

**22. KAREMBO:** **(SHOCKED BY MUM'S REACTION)**
Kuna nini mama? Mbona hasira nyingi?sijawahi kukuona ukiwa hivi.

**23. BETTINA:** Usitie shaka mwanangu... hebu tupumzike kidogo hapa chini ya huu mti.. zawadi bado amelala? kwa sababu yeye hupenda raha sana kama paka wa dukani... ukimtia mbelekoni tu yuwalala.

**24. KAREMBO:** Bado yuasinzia (**TAKES A BREATH)** natamani ningelikuwa mchanga kama yeye.. ndio nibebwe

kila niendako... najisikia mnyonge hata naweza kupeperushwa na upepo kama unyoya...

**25. BETTINA:** Kuwa mkakamavu... kila kitu kitakuwa sawa...

**NARRATOR:**Hivyo basi betina na wanawe karembo na zawadi waliketi chini kupumzika.. betina alitatizwa sana na yale aliyoamulia kutenda... alimdanganya masika mumewake kuwa anakwenda sokoni kununuwa vitu fulani alivyohitaji... hii ndiyo sababu eti alimtaka karembo kwenda naye kumsaidia... lakini azma yake ilikuwa kuwapeleka karembo na zawadi kwa mganga mizanja iliwakaaguliwe... hii ilikuwa mara yake ya kwanza kufanya hivi tena baada ya kushawishiwa na mamake david.. kule mtoni masika alipata habari za kutatanisha...

**SCENE THREE: AT THE LAKE**

**26. C-SFX: WAVES SPLASHING GENTLY ON SHORE**

**27. YAKUBU:** **(CALLING OUT)**
Masika! Wee! Masika!

**28. D-SFX: FEET SPLASHING RAPIDLY IN WATER**

**29. MASIKA:** Yakubu! Hebu aste! aste! Utawafukuza samaki... kuna nini?

**30. YAKUBU:** Nimekuja kukushukuru mwenzangu... asante sana...

**31. MASIKA:** **(PUZZLED)**

Sikuelewi... shukurani za nini?

**32. YAKUBU:** Masika, ulinitoa taka masikioni nilipokuona ukiitumia neti ya mbu kwa kuvulia samaki, Unajuwa nilifanya nini?

**33. MASIKA:** Hapana!

**34. YAKUBU:** Ndiyo! (**EXCITED)** niliichukuwa neti ya mke wangu... na siku hizi sikosi vitoweo... hivi sasa wavuvi wote wa Ribo wanakuiga wewe, wamezitupa neti zao kuukuu na kuzibadili na hizi za kujikingia mbu..

**35. MASIKA:** **(UTTERLY SHOCKED)**
Haiwezekani! Hapana! Eti wavuvi wote?

**36. YAKUBU:** Haswa! hizi neti bwana ni kama zina miujiza ama..

**37. MASIKA:** Hapana! Hivyo si sawa, Sijui nimewashawishi nini...

**38. YAKUBU:** Mbona unajihukumu na umewafaa wavuvi wenzako bwana... na kwa hilo twakupa shukurani!!!

**39. MASIKA:** Hauelewi...nyoye hamuelewi katu! Hebu nikufahamishe kitu...njoo...

**40. D-SFX: FEET AGAIN MOVING RAPIDLY IN WATER**

**41. MASIKA:** Mtazame huyu samaki.... unaona kitu chochote?

**42. YAKUBU:** Ndio..si ni samaki!

**43. MASIKA:** Acha mzaha Yakubu.
(**SERIOUSLY)**
huoni kuwa hawa samaki wote niliowanasa ni wadogo watupu?

**44. YAKUBU:** Sawa, lakini heri nusu shari kuliko shari kamili... ni wadogo lakini ni samaki.. sio kama kukosa!!

**45. MASIKA:** Hapana! Neti hizi zilitengenezwa makhsusi kwa kuzuia mbu wasipite kuwauma wale waliolala chini yake lakini sio kwa ajili ya kuvulia samaki...huoni zina mashimo madogo tofauti na neti zetu za uvuvi,tukiendelea kuvua nazo tutapunguza idadi kubwa ya samaki kwa wingi. mimi nilikosea lakini makosa mawili hayaungi sawa moja..

**46. YAKUBU:** Sote twataka kulisha jamii zetu.. la sivyo hatungelirauka kuja huku ziwani kama sio tamaa... iwe neti hizi ni za mbu au mbayuwayo... mimi sijali... kila la heri katika uvuvi wako... kwaheri..

**47. E-SFX: FOOTSTEPS WALKING ON SAND**

48. **MASIKA:** La! Yakubu! Hebu subiri.. tafadhali subiri..

**NARRATOR:** Wakati mwengine yale tuyatendayo pasipokujuwa ni hatia huweza kuwaathiri watu wengi... masika alijutia lile pato lake la samaki kwa kuwa lilitishia idadi ya samaki na baya zaidi kuwaacha wakaazi wengi bila kinga ya neti zao walizozihitaji... kwengineko, mganga mizanja aliwakaribisha wateja wake kwa mbwembwe kama ilivyo ada yake...

## SCENE FOUR: AT MIZANJA'S SHRINE

**49. (MIZANJA SINGING/CHANTING IN A LOCAL LANGUAGE)**

**50. F-SFX: SHAKERS AND TRADITIONAL JINGLES BELLS**

**51. MIZANJA:** **(AFTER BLOWING IN AIR)**
Hapa ninaona... watoto wako wote wamevamiwa na pepo mbaya anyewanyonya damu na nguvu zao...

**52. KAREMBO:** **(IN HUSHED WHISPER)**
Mama.. mimi naogopa..

**53. BETTINA:** Sssh, Karembo, hebu muwache amalize

**54. KAREMBO:** Mama nimeshikwa na haja ndogo,nahitaji kuenda msalani.

**55. BETTINA:** Hivi sasa?,Karembo..

**56. MIZANJA:** Kimya! Sitaki kusikia sauti yeyote isipokuwa ya mizimu yangu... subirini hapa naja!

**57. (MIZANJA EXITS WITH SAME CHANTING/SINGING)**

**58. BETTINA:** Haya nenda nje haraka! Na ukimaliza urudi kabla hajarudi. Haya haraka!!!

**59. G-SFX: BABY/ZAWADI STARTS TO CRY**

**OUTRO/NARRATOR: K**arembo keshapata fursa aliyotaka.. alijikokota taratibu na kuondoka katika pango la mizanja. Hakujali hasira za mamake atakapogunduwa katoweka. Lakini, anakwenda wapi? Atafaulu kweli? Ni matibabu gani mizanja atakayompa zawadi? Je, masika atafanya nini akitambuwa kuwa neti za mbu zinafanyiwa ubadirifu na wavuvi wenzake? Kuyabaina haya, basi usikose kujiunga nasi tena katika mchezo wa kuigiza kwa jina WA**GENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA DHIDI YA MALARIA"** unapotaka kusikiza tena au kutuma maoni yako tembelea tovuti zetu www.dw-world.de/lbe

Hadi wakati mwengine..Kwaheri.